NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

25 Novemba 2020

Kwa Wabahá'í wa Ulimwengu

Marafiki wapendwa sana,

Tunawasalimu kwa upendo mwingi kwenye siku hii maalum, tukio la kukumbuka nguvu ya Agano, ile nguvu ambayo "hurindima katika mwili wa ulimwengu wa nasibu" na huendeleza mbele vifungo vidumuvyo vya upendo miongoni mwa waumini. Miezi kadhaa tangu Riḍván, tumeona shuhuda za nguvu hii yenye uwezo katika shughuli unganishi za wafuasi wa Bahá'u'lláh, zikiongozwa kwa ustadi mkubwa na asasi za Hoja katika kila bara na nchi, kadiri ambavyo marafiki kila mahali wametafuta kwa sifa bainifu ubunifu na dhamiri kusimamia mahitaji ya ulimwengu utaabikao. Ustahimilivu wenu na msimamo wenu usioyumba kwenye ustawi wa wale wanaowazunguka, ulioendelea kuwepo katika shida zote, umetujaza matumaini makubwa mno. Lakini haishangazi kwamba, katika baadhi ya mitaa, matumaini yamekuwa rasilimali haba. Kuna utambuzi uongezekao kwa upande wa watu wa ulimwengu kwamba miongo kadhaa ijayo itakuja/italeta pamoja nayo changamoto ambazo ni za kutisha kabisa ambazo familia ya binadamu haijapata daima kukabiliana nazo. Janga la kiafya la sasa la ulimwengu ni mojawapo tu ya changamoto hizo, ukali wa mwisho wa gharama yake, kwa vyote viwili uhai na njia za kujipatia riziki, bado haufahamiki; jitihada zenu za kuauniana na kusaidiana mmoja kwa mwingine hali kadhalika dada na kaka zenu katika jamii kwa jumla kwa hakika zitahitaji kuendelezwa, na sehemu nyingine kupanuliwa.

Ni dhidi ya usuli huu wa dhoruba zenye ghadhabu zinazoipa kichapo jamii ya binadamu kwamba safina ya Hoja inakaribia kuanzisha mfululizo wa Mipango ambayo itaipeleka hadi kwenye karne ya tatu ya Zama za Kibahá'í na kwa umuhimu kuimarisha kwa namna kubwa sana uwezo wa jumuiya ya Kibahá'í katika kuleta nguvu za ujenzi wa jamii za Imani. Kama mtambuavyo, Mpango wa kwanza utakaoanzisha mfululizo huu mpya utadumu kwa mwaka mmoja tu. Pale ambapo mazingira yatazizuia jumuiya za kitaifa kuanzisha programu za ukuaji wa nguvu nyingi iwezekanavyo kabla ya Riḍván 2021 kama zilivyodhamiria, miezi hii kumi na mbili itarefusha muda zilio nao kufanya hivyo. Wakati huo huo, popote ambapo mchakato wa ukuaji tayari umezidishwa nguvu, mwaka huu mmoja utakuwa ni fursa ya kuimarisha mafanikio yaliyopatikana wakati wa Mpango wa sasa, wakati zikijenga mazingira muhimu kwa ajili ya kukaribisha idadi kubwa zaidi na zaidi ya roho katika mkumbatio wa jumuiya itambulikayo kwa ushupavu wake na muelekeo wake wa kutizama nje. Katika ngazi za kitaifa, kikanda na klasta, tunatarajia jumuiya zenye nguvu iliyothibitishwa ziwasaidie wale ambao tajiriba kidogo imeongezeka. Katika jitihada hii ya mwaka mzima, kila jumuiya lazima ichote uwezo wowote inaoweza kuwa nao ambao bado haujatumika na kutafuta kuvishinda vikwazo ambavyo vinazuia ukuaji wake, hapo kuiandaa kwa ajili ya mahitaji yajayo. Kwa kuwa ni katika muktadha wa jumuiya inayoshamiri, hasa ile ambayo ni kiini cha shughuli shadidi katika kijiji au ujirani, na pale ambapo kila kipengele cha muundo wa Mpango kimepewa uangalifu inaouhitaji, kwamba

vipengele hivyo hufungamana na kuungana kwa uwazi zaidi, huzidisha uwezo wa jumuiya katika uga wa huduma.

Mbali na kuleta maendeleo ndani ya klasta kila mahali, Mpango ujao utakuwa ni mwaka wa tafakari ya kina juu ya maisha ya ‘Abdu’l-Bahá na uimara wa Agano ambapo Yeye alikuwa ni Kiini, wakati jumuiya inapojiandaa kuadhimisha miaka mia moja ya Kupaa Kwake. Maadhimisho ya siku hii ya ukumbusho bila shaka yatawachochea watu binafsi na jumuiya kadhalika kutafakari maana ya kitambo kile chenye kutia uchungu usio na mwisho ambapo Yule Ambaye alikuwa Fumbo la Mungu alipoondoka hapa ulimwenguni. Kufariki Kwake kuliwanyang’anya Wabahá’í wa enzi hizo Mtu Ambaye alikuwa ndiyo kusudi la upendo wao na uaminifu wao wa kina; kwa waaminifu wa kipindi hiki, Yeye anabakia asiyelinganishwa: mfano mkamilifu wa wema halisi kwa maneno na vitendo wa yale yote ambayo Baba Yake alifundisha, Yule Ambaye kupitia Yeye Agano la Bahá’u’lláh “lilitangazwa, kutetewa na kuthibitishwa”. Tunatambua kwamba mwaka ujao pia utaashiria karne moja tangu Wasia na Agano Lake—ule Waraka wa “maana sana”, wa “kihistoria”, wa “milele”—"ulioletwa kwenye uhai, kuelezea sura na kuanzisha michakato” ya Utaratibu wa Kiutawala, “muundo hasa wa ule ustaarabu mtakatifu ambao Sheria ya Bahá’u’lláh yenye nguvu imekusudia kuuanzisha duniani”. Utaratibu huu wa “kipekee” na “uliotiwa utakatifu” huu “muundo wa kiutawala wenye nguvu”, ulikuwa umeundwa na Muasisi wake ili kudumisha Agano na kuzielekeza nguvu za kiroho za Hoja. Itakuwa dhahiri, basi, kwamba Siku ya Agano mwaka ujao, miezi kumi na mbili kamili kutoka sasa, itakuwa na maana hasa. Tunayaomba Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa kuamua jinsi gani tarehe hizi mbili, zinazotokea pamoja kwa karibu, kila moja iweze kuadhimishwa, ikizingatiwa hali zilizopo katika nchi zao.

Wakati wote, maandalizi yenye ari yanaendelea kufanywa katika Nchi Takatifu kwa ajili ya maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka mia moja ya Kupaa kwa ‘Abdu’l-Bahá kwenye mkusanyiko ambao, inatumainiwa, wawakilishi wa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa na Halmashauri za Kibahá’í za Kanda watakuwepo. Vivyo hivyo, mipango tayari inafanywa kwa ajili ya kongamano la Bodi za Washauri wa Bara na Washauri Wasaidizi, ambapo litafanyika wakati mmoja, hapo Januari 2022, na kupita kwa miaka mia moja tangu usomwaji wa kwanza hadharani wa Wasia na Agano la Bwana. Hali iliyopo ulimwenguni inaweza, hata hivyo, kuhitaji mipango inayofanywa kwa ajili ya mikusanyiko hii kwenye Makao Makuu ya Ulimwengu ya Imani ya Kibahá’í` kubadilishwa. Lakini hata iweje, hatuna shaka kwamba jitihada zinazofanywa katika jumuiya za mahali kote ulimwenguni ili kuadhimisha ifaavyo Kupaa kwa ‘Abdu’l-Bahá na kuienzi Siku ya Agano katika mwaka huu ujao wa kumbukumbu ya miaka mia moja zitatoa kichocheo kihitajikacho kwa ajili ya kuzindua hatua ifuatayo katika Mpango Mdogo wa Mungu, kama ambavyo Majaliwa husukuma ukunjukaji wa Mpango Wake Mkuu kulingana na amri Yake isiyopingika.

Nguvu ya uhakika itakayojenga kila duru chanjari la Mpango wa Mwaka Mmoja itazidishwa zaidi kwa kuachiliwa kwa filamu mbili. Ya kwanza kati ya hizi, ambayo itapatikana kwa wakati kwa ajili ya maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka mia moja, itakuwa ni taswira ya Nafsi ya ‘Abdu’l-Bahá. Mbali na kuwa shukrani kwa maisha na kazi Zake, itachunguza namna gani, kwa kupigania umoja wa binadamu kupitia maneno na matendo Yake, alivyotoa changamoto kwa dhana za ovyo na chuki za enzi zile, na kutoa kichocheo kwenye mchakato wa uunganishaji ambao unaendelea

hadi leo. Filamu ya pili, itakayofuata punde tu baada ya ile ya kwanza, itaakisi juu ya kumalizika kwa miaka mia moja ya kwanza ya Zama za Utungo ikitazamwa kutoka kwenye vilele ambapo jumuiya ya Kibahá'í imepanda, na kutoka mahali ambapo sasa inaweza kutazama peo mpya.

Umuhimu wa matukio haya yanayoadhimishwa wakati wa Mpango wa Mwaka Mmoja utaipa sifa za kipekee, kuendeleza kazi inayofanywa katika klasta na kuufanya mwaka huu mmoja kuwa maandalizi bora kwa ajili ya jitihada ya kiulimwengu ambayo itafuata. Tukiwa na hisia yenye matarajio ya furaha, tunatangaza kwamba Ulimwengu wa Kibahá'í, wakati wa Riḍván 2022, utaanza Mpango wa Miaka Tisa. Mahitaji na maelekezo yake yatatolewa hapo baadaye, lakini muda wake tayari unatupa ishara isiyo na shaka ya matazamio ya utanuzi itakayotoa. Mungu akipenda, itatanguliwa na mkutano wa mfululizo wa makongamano itakayofanyika katika kipindi cha miezi kadhaa kote ulimwenguni.

Hii, kama inavyoweza kutarajiwa hadi sasa, ni njia ambayo jumuiya ya Kibahá'í itataka kuikanyaga. Kwa saa hii, tunawasihi kujifunga tena nguvu zenu, mkijikita kwenye kazi maalum ya haraka iliyopo mbele yenu. Tumefurahishwa kwa kiasi kikubwa kuona utulivu uliohakikishwa ambao kwao jumuiya ya Jina Kuu Kabisa imetafuta kutoa tiba takatifu katika hali zote, hususan katika wakati huu ambapo mitindo ya maisha ya jamii iliyojikita mizizi imevurugwa na hatari za aina mbalimbali inawakabili wengi sana. Aidha, marafiki lazima wawe waangalifu dhidi ya kuvutwa kwenye hatma ya migogoro na ugomvi visivyo na manufaa ambavyo ndivyo huyapambanua sana majadiliano ya shughuli za jamii, au—Mungu aepushilie mbali—kuruhusu maingiliano ya aina hii, hata kwa muda mfupi tu, kupenyeza katika mazungumzo ya jumuiya. Hata hivyo hadhari kama hiyo kwa upande wenu katika kujiepusha na kutoelewana na kutozongomezwa katika mabishano ya kijamii haipaswi kwa hali yoyote ile kutafsiriwa kama kujitenga kutoka mambo mengi ya haraka ya wakati huu. Ni mbali na hili. Ninyi ni miongoni mwa watendaji hai na wenye bidii mno kati ya watakia heri wa jamii ya binadamu. Lakini, ama kupitia matendo au maneno, ustahili wa kila mchango wenu kwa ajili ya ustawi wa kijamii umo, kwanza, katika uthabiti wa kujifunga kwenu kugundua ile sehemu ya thamani kubwa ya umoja ambapo mitazamo inayotofautiana huingiliana na ambayo kwayo watu wanaopingana wanaweza kuungana.

Ni chini ya duru mbili kamili zimebakia za Mpango wa Miaka Mitano wa sasa—hakika, kati ya mfululizo wa sasa wa Mipango uliozinduliwa mnamo 1996. Katika miezi hii ya mwisho, tutakuwa na hakika kutoa sala za shauku kwa niaba yenu katika maombi yetu kwenye Kizingiti Kitakatifu. Muweze kufanikiwa katika kuwapa matumaini wale ambao hawajui wapi pa kuyapata katika ulimwengu unaokanganya na unaoyoyoma, kwa sababu tu ya kukosa umoja ambao ninyi, kupitia ibada yenu ya moyo mliyoahidi kwa Agano, umedhihirishwa wazi wazi kabisa.

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu